BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA SABA

Kikao cha Tano – Tarehe 03 Disemba, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Kamisheni ya Utumishi wa Umma juu ya Hali na Ufanisi wa Utumishi wa Umma Zanzibar kwa mwaka 2023/2024.

**Wizara ya Afya:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Wizara ya Afya kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar (ZFDA) kwa mwaka 2023/2024.

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Wizara ya Afya kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar kwa mwaka 2023/2024

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Kamisheni ya Utumishi wa Umma juu ya Hali na Ufanisi wa Utumishi wa Umma Zanzibar kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar (ZFDA) kwa mwaka 2023/2024.

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar kwa mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:**

86. MHESHIMIWA CHUM KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

    Kwa kuwa suala la uhifadhi wa mazingira ni suala mtambuka.

    Je, ni kwa kiasi gani taasisi mbali mbali zinachukua hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanayotokana na matumizi mabaya ya mazingira.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

124. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    Mkataba wa Kimataifa Na. C190 unalenga kupinga ukatili wa kijinsia mahali pa kazi, ukiwa ni mkataba jumuishi unaohusisha wafanyakazi wote, sekta rasmi au zisizo rasmi, vijijini na mijini. Mkataba huu ni muhimu kwa mustakabali wa kuondoa ukatili wa kijinsia mahali pa kazi.

    (a) Ikiwa Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni sababu gani za msingi zilizoifanya nchi yetu kushindwa kuuridhia mkataba huu mpaka leo.

    (b) Je, kwa sasa hali iko vipi juu ya unyanyasaji wa kijinsia katika sekta rasmi na zisizo rasmi hapa Zanzibar.

    (c) Ni miongozo ipi inayotumika kutatua kesi za unyanyasaji wa kijinsia katika maeneo ya kazi.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

108. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwepo na ongezeko kubwa la mabango yanayowekwa katika barabara kuu yanayotangaza biashara za kampuni na taasisi binafsi. Jambo hili limeleta mkanganyiko mkubwa kwa wananchi ambao hawafahamu utaratibu na makusanyo ya kodi katika mabango hayo.

(a) Ni utaratibu gani unaotumika kuweka mabango katika barabara kwa ajili ya biashara na matangazo.

(b) Ni mabango mangapi yamewekwa katika barabara kuu kwa matangazo ya kibiashara.

(c) Ni mapato ya kiasi gani hukusanywa kwa mwaka kupitia uwekaji wa mabango katika barabara kuu.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

9. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kumekuwa na malalamiko makubwa kutoka kwa wastaafu kuhusu utofauti katika ukokotoaji wa mafao ya kiinua mgongo na pensheni kutokana na tofauti za mfumo wa ukokotoaji unaotumika kati ya Wizara yako na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF).

(a) Je, kwa kiasi gani Serikali inaitambua changamoto hii na ni hatua gani imechukuwa kuitatuta.

(b) Je, ni mfumo upi wa ukokotoaji wa mafao kwa wastaafu unatumika hapa Zanzibar.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka uwiano na umoja katika mifumo hii ya ukokotoaji ili kuondoa malalamiko haya na kuhakikisha haki kwa wastaafu inapatikana.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

47. MHESHIMWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

    Ni utaratibu gani unaotumika mpaka kufikia maamuzi ya baadhi ya vitabu vya fasihi ya Kiswahili na fasihi ya Kiengereza kukubalika kufundishwa maskulini.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

36. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

    Kiswahili kwa sasa ni hazina yenye thamani kubwa Tanzania, Afrika na dunia kwa ujumla.

    Je, Wizara inachukua hatua gani za kinidhamu kwa baadhi ya wasanii wanaojaribu kukizungumza Kiswahili hususani Kiunguja Mjini kwa njia ya kukikebehi na kukifanyia mzaha katika ladha ya matamshi yake.

37. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

    Licha ya kuingia katika mageuzi mapya ya habari bado wananchi wengi wana shauku ya kurejea kuziona tamthilia za zamani, zikiwemo za Mashaka, Halikuniki, Sekembuke, Dkt. Ayoub na nyenginezo.

    (a) Je, ni ipi kauli ya Wizara yako kupitia ZBC katika kusikiliza kilio hiki cha wapenzi wao.

    (b) Ni kwa kiasi gani tamthilia hizi zimeweza kuhifadhiwa vyema kwa maslahi ya kuuenzi utamaduni wetu.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

121. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kumekuwepo na malalamiko ya muda mrefu kuhusu kuchelewa kutoa hatimiliki za uhaulishaji wa ardhi. Kuchelewa huko kumesababisha wananchi wengi kupoteza imani na Kamisheni ya Ardhi katika utoaji wa hatimiliki.

(a) Ni sababu zipi zinazochangia kuchelewa kutoa hatimiliki za ardhi.

(b) Kwa mujibu wa sera na sheria, ni muda gani mchakato wa kutoa hatimiliki unapaswa kukamilika.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kulitatua tatizo hili ambalo lipo kwa muda mrefu bila ya kutatuliwa.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

28. MHESHIMWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

(a) Kwa mujibu wa takwimu tunahitaji kuzalisha lita ngapi za maji zitakazowatosheleza wananchi wetu kwa matumizi yao ya kila siku.

(b) Je, ni lita ngapi za maji zikiwa kama ni benki ya maji, zinahitajika kutunzwa ili kuweza kuwatosheleza wananchi wetu kwa matumizi yao ya baadae.

(c) Ni yepi matarajio ya kuzifikia lita hizo kwa ujumla wake.

**Wizara ya Afya:**

22. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Je, Serikali imefanya tathmini au tafiti yoyote juu ya faida na madhara ya chanjo za nyembe na vijembe wanazotumia waganga wa tiba asilia kwa wananchi wanaofika kupata huduma za kimatibabu.

111. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Pamoja na juhudi za Serikali katika kujenga Hospitali ya Kinyasini kwa wananchi wa Wilaya ya Wete, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi juu ya kukosekana kwa eneo la kusubiria wagonjwa katika Hospitali hiyo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga eneo la kusubiri wagonjwa katika Hospitali ya Kinyasini na hospitali nyengine zenye matatizo kama haya.

(b) Je, Serikali imefikia hatua gani katika ujenzi wa Hospitali ya Wete, ambayo kwa sasa vitengo vingi vimehamishiwa Hospitali ya Kinyasini.

<u>**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**</u>

71. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Wananchi wa Mwanakwerekwe wanaishukuru Serikali ya Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa shughuli inayoendelea hivi sasa ya uchimbaji wa misingi ya mitaro ya maji katika barabara za ndani.

Ni kwa kiasi gani changamoto ya kukatwakatwa kwa mabomba ya maji itarekebishwa ili kuwaondolea wananchi usumbufu wa kukosa huduma ya maji safi na salama.

<u>**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**</u>

16. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Tathmini ya utekelezaji wa mikakati ya kilimohai ipo katika sura ipi kwa sasa.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

122. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Pamoja na juhudi za taasisi za Serikali katika utoaji wa huduma za kijamii, bado kuna changamoto nyingi zinazopelekea kushindwa kufikia viwango vya kimataifa katika kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali kulingana na Kiwango cha Ubora wa Kimataifa (ISO 9001:2015).

(a) Je, ni taasisi ngapi zimepata uthibitisho wa kufuata viwango vya Kimataifa (ISO) Zanzibar.

(b) Ni masharti gani ambayo taasisi zinatakiwa kuyakidhi ili kupata uthibitisho wa Kimataifa (ISO) katika utoaji wa huduma.

(c) Ni mpango upi wa Serikali wa muda mrefu unaohakikisha kuwa taasisi zinapata uthibitisho wa Kimataifa (ISO) katika utoaji wa huduma.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

61. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

(a) Kwa kiasi gani vijana wanaopiga mbizi maarufu kama makachu waliopo Forodhani, wanaendelea kuitangaza vyema Zanzibar kupitia sekta ya Utalii.

(b) Ni watu gani miongoni mwa watu mashuhuri walioonesha kuvutiwa na mtindo huo na hata wengine kuweka nia ya kuitembelea Zanzibar.

(c) Je, matarajio ya Serikali ya kuwaweka vijana hawa katika mazingira bora zaidi yamefikia wapi.

62. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Tanzania ni miongoni mwa nchi tano Afrika zinazopokea uwekezaji mkubwa katika sekta ya utalii.

(a) Ni mambo gani ya msingi ambayo mataifa mengine duniani yanaweza kutuiga.

(b) Ni aina gani ya utalii inayowavutia watalii wengi duniani kuitembelea Zanzibar.

(c) Je, Zanzibar inasimama kama ni nchi ya ngapi kwa mwaka huu katika nchi za Afrika kwa kupokea idadi kubwa ya watalii.

## III. TAARIFA ZA SERIKALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Kamisheni ya Utumishi wa Umma juu ya Hali na Ufanisi wa Utumishi wa Umma Zanzibar kwa mwaka 2023/2024.

**Wizara ya Afya:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Wizara ya Afya kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar (ZFDA) kwa mwaka 2023/2024.

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Wizara ya Afya kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar kwa mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**03 Disemba, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**